

# SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Simu: 2133990  
Telegramu: Railways  
Nukushi: 2133428



Ofisi ya Uhusiano TRC  
S.L.P 76569  
Dar es Salaam

---

## TAARIFA KWA UMMA

### KAMPENI YA USALAMA WA RELI KWA KUZUIA AJALI, UHARIBIFU NA HUJUMA

**Dare es Salaam, Januari 28, 2020**

Shirika la reli Tanzania – TRC limeandaa kampeni maalum ya kutoa elimu ya uelewa kuhusu usalama katika reli ili kuepusha ajali, uharibifu na hujuma katika miundombinu na kusababisha vifo, majeruhi, na hasara itakayotokana na ulazima wa kutengeneza treni na njia ya reli.

TRC leo tunazindua kampeni ya usalama katika reli ambapo TRC inawaomba wanachi, taasisi zisizo za Ki-Serikali, viongozi wa Serikali kutoka ngazi ya vijiji mpaka Mkoa na Taifa pamoja na wana-Siasa, kwa pamoja tunaguswa na madhara ya kukosekana kwa usalama katika reli kwani ajali ikitokea itakuhusu wewe binafsi, ndugu, rafiki ama m-Tanzania mwenzio.

Ili tuweze kuimarisha usalama katika reli inapasa kila mwananchi na mdau kwa nafasi yake awe mmstari wa mbele kuhakikisha kwamba yafuatayo yanafanyika;

- Madereva wa magari, pikipiki na baiskeli wawe waangalifu wanapo elekea kukatisha vivuko vya reli
- Muhimu kuheshimu alama zote zilizowekwa kwenye makutano ya barabara na reli
- Kulinda vifaa vya miundombinu ya reli kwa kujiepusha na wizi pamoja na kutoa taarifa ya viashiria vya mtu yeyote anayehujumu au kuiba kifaa chochote cha reli.
- Kujiepusha na uharibifu wa mazingira unaopelekea miundombinu ya reli kuharibiwa na maji ya mvua. Wananchi wajiepushe kufanya shughuli za kijamii pembezoni mwa reli, kwenye hifadhi yote ya ardhi ya reli ya mita 60 njiani, kwenye mipaka ya stesheni pamoja na karibu na kingo za mito.
- Kutoa taarifa ya viashiria vyovyote vinavyo weza pelekea kuathiri USALAMA WA RELI vilivyoelezwa hapo juu.

Tunatoa rai kwa wananchi, madereva wote wa vyombo vitembeavyo barabarani, wanaoishi kando kando ama kusafiri katika ushoroba wa maeneo ambako reli ya TRC inapita na kuna vivuko vya reli, katika mikoa yote Tanzania kwa kuzingatia usalama wa reli.

Pamoja na mikoa mingine, naomba kusesitiza kuwa baada ya TRC kuanza kupeleka treni za abiria na mizigo Moshi, wananchi na madereva wanaosafiri katika mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, na Arusha wawe makini zaidi kwa kuwa njia hiyo iliacha kutumika kwa muda mrefu na kupelekea wananchi kutofuata taratibu na sheria hasa katika makutano ya barabara na reli.

Mara kadhaa kumekuwa na matukio ya baadhi ya wananchi wasio raia wema wanajaribu kuiba ama kufanya hujuma kwa kutega vyuma relini. Serikali inatambua katika maeneo hayo wanako jaribu kuhujumu ama kutega treni, wapo raia wema. Ili kujiepusha na adha itakayotokana na utekelezaji za kuwasaka wahalifu hao, ni vyema raia wema watoe ushirikiano kwa kutoa taarifa kwenye vyombo vya usalama ama viongozi wa Serikali kuanzia na ngazi ya vijiji.

Aidha elimu hii inayotolewa, tushirikiane kutoa elimu hii kwa jamii inayotuzunguka, ili kulinusuru taifa na majanga ya ajali relini pamoja na uharibifu na hujuma kwenye minudombinu ya reli maana reli hii ni mali ya watanzania na imefufuliwa kwa fedha za walipa kodi watanzania.

TRC tunaamini mlinzi namba moja wa nchi ni mwananchi hivyo, hima tushiriki kwa kuzingatia usalama pamoja na kuepusha uharibifu na hujuma kwenye reli.

kupitia fursa hii napenda kutambulisha mawasiliano ya simu ya NAMBA YA BURE ambayo raia yeyote mwema ataweza kuitumia kutoa taarifa bila kubughudhiwa;

**NAMBA YA BURE NI: 0800110042**

**RELI YETU, MAENDELEO YETU, TAIFA LETU**

---



**Imeandaliwa na Mkuu wa kitengo cha Uhusiano TRC**

**Jamila Mbarouk**